# Zahabu SAFI

Scriptures taken from Biblia, Kitabu cha Mungu.
Copyright © Everyday Publications Inc.

# Maneno kutoka kwa Biblia, maandiko Matakatifu, Ni Neno la Mungu.

Edition 2021
© by GBV
printed in Germany

**GBV Dillenburg GmbH**
Eiershäuser Straße 54
35713 Eschenburg
GERMANY
www.gbv-dillenburg.de
www.gbv-online.org

Katika Mwanzo
alikuwa Neno,
na Neno alikuwa
pamoja na Mungu,
na Neno alikuwa Mungu.

*Yoane 1:1*

Ndani yake
alikuwa uzima,
na uzima alikuwa
nuru ya watu.

*Yoane 1:4*

Basi Yesu
akasema nao tena:
“Mimi ni nuru ya dunia;
yeye ambaye ananifuata
hatakwenda kwa
giza kabisa,
lakini atakuwa na
nuru ya uzima.”

*Yoane 8:12*



“Mimi ndimi njia,
na kweli,
na uzima:
mtu hakuji kwa Baba,
ila kwa mimi.”

*Yoane 14:6*

Yesu akapaza sauti yake,
akisema “Mtu akion
kiu aje kwangu, anywe.
Yeye anayeamini mimi
kama maandiko
yalivyosema,
mito ya maji ya uzima
itatoka tumbo lake.”
*Yoane 7:37-38.*



“Kujeni kwangu,
ninyi wote
munaosumbuka
na wenye mzigo
mzito, name
nitawapumzisha ninyi.”
*Matayo 11:28*

“Kwa maananira
yangu ni laini,
na mzigo
wangu ni mwepesi.”
*Matayo 11:30*

“Mungu
unirehemu mimi
mwenye zambi”

*Luka 18:13*

Kwa maana mshahara
wa zambi ni mautu,
lakini zawadi ya Mungu
ni uzima wa milele katika
Yesu Kristo Bwana yetu.

*Waroma 6:23*



Yesu akajibu
akamwambia,
“Ila mtu azaliwe mara
ya pili hawezi kuona
ufalme wa Mungu.”

*Yoane 3:3*

“Usishangae
kwa sababu nilikuambia,
‘sharti muzaliwe mara
ya pili.’”

*Yoane 3:7*

Tubuni basi, mugeuke,
ili zambi zenu ziondoshwe.
*Matendo ya Mitume 3:19*

Tukikiri zambi zetu,
yeye ni mwaminifu
na wa haki hata
atuondoleezambi zetu,
na kutusafisha na
uzalimu wote.
*1 Yoane 1:9*



Lakini wote
ambao walimpokea
aliwapa uwezo wakuwa
watoto wa Mungu,
ndio wale walioamini
Jina lake: waliozaliwa
... kwa Mungu.
*Yoane 1:12-13*

"Kweli kweli
ninawaambia ninyi,
Yeye anayesikia
neon langu na
kumwamini yeye
ambaye alinituma,
ana uzima wa milele;
hafiki kwa hukumu,
lakini amepita kutoka
mauti kuingia uzima."

*Yoane 5:25*



"Kwa maana
Mungu alivyopenda
ulimwengu,
hata kutoa Mwana
wake wa pekee,
ili kila mtu
akimwamini asipotee,
lakini apate uzima
wa milele. "

*Yoane 3:16*

Lakini aliumizwa
kwa makosa yetu,
Alichubuka kwa
maovu yetu.
Azabu ya salama
yetu ilikuwa juu yake,
na kwa kupugwa Kwake
sisi tumepona.
*Isaya 53:5*



"Tazama ninasimama
kwa mlango,
ninapiga hodi;
kama mtu akisikia
sauti yangu na kufungua
mlango, nitaingia kwake. "
*Ufunuo 3:20*

Kristo akae ndani
ya mioyo yenu kwa imani.
*Waefeso 3:17*

"Maana Mwana
wa watu alikuja kutafuta
na kuokoa yule ailyepotea. "

*Luka 19:10*

"Naye anayekuja
kwangu sitamtupa
inje kabisa."

*Yoane 6:37*



Kujeni,
kwangu vitu vyote ni tayari.

*Luka 14:17*

Bwana zangu,
nifanye nini
nipate kuokolewa.
Amini Bwana Yesu Kristo,
nawe utaokolewa.

*Matendo 16:30-31*

Kwa jina Lake kila
mtu ambaye anamwamini
atapewa usamehe wa zambi.

*Matendo ya Mitume 10:43*

Yesu Bwana wetu ...
aliyetolewa kwa
ajili ya makosa yetu,
na kufufuliwa
ili tuhesabiwe haki.

*Waroma 4:24-25*



Sasa, basi hakuna
hukumu ya azabu juu yao
walio katika Yesu Kristo.

*Waroma 8:1*

Ninawaandikia
ninyi wenye kuamini
Jina la Mwana wa Mungu,
maneno haya,
ili mujue ya kuwa muna
uzima wa milele.

*1 Yoane 5:13*

"Furahini kwa
sababu majina
yenu yameandikwa
katika mbingu. "

*Luka 10:20*

Basi tukikwisha
kuhesabiwa haki kwa
njia ya imani,
tuna salama kwa
Mungu kwa njia ya
Bwana wetu Yesu Kristo.

*Waroma 5:1*



Kwa maana
mumeokolewa kwa neema
kwa njia ya imani, wala
neno hili halikutoka ndani
yenu wenyewe, ni zawadi
ya Mungu, si kwa matendo
asiwe mtu atakayejisifu.

*Waefeso 2:8-9*

Mungu ashukuriwe
kwa sababu ya zawadi
yake tusioweza kuisifu
kama inavyopasa!

*2 Wakorinto 9:15*

Lakini kama
tukitembea katika nuru,
kama yeyealivyo katika nuru,
tunashirikiana sisi kwa sisi,
na damu yake Yesu,
Mwana wake,
inatusafisha zambi zote.

*1 Yoane 1:7*



"Kondoo zangu
wanasikia sauti yangu,
nami ninawajua nao
wananifuta,
nami ninawapa uzima
wa milele,
nao hawatapotea
hata milele,
wala hakuna
mtu anayeweza
kuwanyanganya toka
mkono wangu. "

*Yoane 10:27-28*

Maana Kristo
aliteswa ka
ajili yenu vilevile
akiwaachia ninyi
mfano mufuate
nyayo zake.
*1 Petro 2:21*



"Na tazama,
mimi ni pamoja nanyi
siku zote hata
mwisho wa dunia. "
*Matayo 28:20*

"Vivyo hivyo nuru yenu
iangaze mbele ya watu,
waone matendo
yenu mazuri,
watukuze Baba yenu
aliye mbinguni.
*Matayo 5:16*

"Sababu kila mtu
atakayeona haya juu
yangu na juu
ya maneno yangu,
Mwana wa watu ataona
haya juu ya mtu huyu
siku ile atakapokuja
katika utukufu wake,
na wa Baba yake,
na wa malaika
watakatifu. "

*Luka 9:26*



Majani yanakauka,
ua linakauka;
Lakini neno la Mungu
wetu litasimama milele.

*Isaya 40:8*

"Heaven and earth
will pass away,
but My words
will by no means
pass away."

*Luke 21:33*

Musijishumbushe
wenyewe kwa neno lo lote;
lakini katika kila neno
kwa kuomba na
kusihi pamoja na
kushukuru maombi
yenu yajulikane na Mungu.
Na salama ya Mungu,
inayopita akili zote,
italinda mioyo yenu na
nia zenu katika Kristo Yesu.

*Wafilipi 4:6-7*



Ndio nimekupenda
kwa mapendo ya milele,
kwa sababu hii
nimekuvuta kwa wema
wa mapendo yangu.

*Yeremia 31:3*

Usiogope
kwa maana mimi ni
pamoja nawe.

*Isaya 41:10*

“Ninakwenda
kuwatengenezea
ninyi pahali.
Na kama ninakwenda
kuwatengenezea
ninyi pahali,
nitakuja tena na
nitawakaribisha
ninyi kwangu;
pahali ninapokaa mimi,
mukae vilevile. ”

*Yoane 14:2-3*



Kwa sababu Bwana
mwenyewe atashuka
toka mbinguni,
na sauti kubwa ...
nao waliokufa katika
Kristo watafufuliwa kwanza;
kisha sisi tulio hai, tuliobaki,
tutanyanyuliwa pamoja
nao katika mawingu,
kukutana na
Bwana katika hewa,
na hivi tutakuwa pamoja
na Bwana milele.

*1 Watesalonika 4:16-17*

Nikaona mbingu mpya
na dunia mpya.
*Ufunuo 21:1.*

Naye atapangusa kila
chozi katika macho yao;
wala mauti haitakuwa tena;
wala maombolezo, wala kilio,
wala uchungu
hautakuwa tena;
kwa maana maneno ya
kwanza yamekwisha pita.
*Ufunuo 21:4*



"Tazama ninakuja upesi."
*Ufunuo 22:12*

Naye mwenye kiu, aje;
na yeye anayetaka atwae
maji ya uzima bure.
*Ufuno 22:17.*

Amina.
Kuja Bwana Yesu.
*Ufuno 22:20*

Soma Biblia, ndilo Neno la Mungu. Sikiliza sauti yake Mungu. Mungu mkubwa aliye hai anakujali. Anataka ujue mapendo yake. Katika Neno Lake, Anakuonyesha njia ya kupumzika kwa kweli, kwa furaha ya kweli na amani.

Kama hauna Biblia tungependa kukutumia Agano Jipya la bure (sehemu ya pili ya Bibilia) ukiomba.

Ukiwa na maswali yoyote tutajaribu kukujibu kwa furaha.

GBV 146 4120 Pure Gold Swahili